

# HALMASHAURI YA MANISPAA YA UBUNGO



14 APRILI, 2021

## TANGAZO

**YAH: KUSUDIO LA KUTUNGA SHERIA NDOGO ZA HALMASHAURI YA  
MANISPAA YA UBUNGO.**

**CHINI YA KUFUNGU CHA 89 CHA SHERIA YA SERIKALI ZA MITAA  
(MAMLAKA ZA MIJI) YA 1982 ILIYOREJEWA MWAKA 2002.**

**MKURUGENZI WA HALMASHAURI YA MANISPAA YA UBUNGO  
ANAWATANGAZIA WANANCHI KUWA HALMASHAURI IKO KWENYE  
MCHAKATO WA KUANDAA NA KUFANYA MAREJEO YA SHERIA NDOGO  
ZA HALMASHAURI ZITAKAZOSAIDIA UENDESHAJI WA HALMASHAURI.**

**HIVYO WANANCHI WOTE WA MANISPAA YA UBUNGO MNAALIKWA  
KUTOA MAONI YENU AU PINGAMIZI KWA MAANDISHI KWA AFISA  
MTENDAJI WA KATA AU MTA A NDANI YA SIKU 14 KUENZIA TAREHE YA  
TANGAZO HILI.**

**RASIMU ZA SHERIA PENDEKEZWA:-**

- i. Sheria ndogo ya Afya na Usafi wa Mazingira ya Mwaka 2021.**
- ii. Sheria Ndogo ya Mfuko wa Elimu ya Mwaka 2021.**

**SHERIA ZINAZOFANYIWA MAREJEO:-**

- i. Sheria Ndogo ya (Ada na Ushuru) ya Halmashauri ya Manispaa ya  
Ubungo ya mwaka 2019. Tangazo la Serikali Na. 223 la tarehe 22/3/2019**
- ii. Sheria Ndogo za (Ushuru wa Huduma) za Halmashauri ya Manispaa ya  
Ubungo ya mwaka, 2019. Tangazo la Serikali Na. 224 la tarehe 22/3/2019**

**RASIMU ZA SHERIA PENDEKEZWA ZINAPATIKANA KWENYE OFISI ZA SERIKALI ZA  
MITAA NA KATA, KWENYE TOVUTI YA HALMASHAURI ([www.ubungomc.go.tz](http://www.ubungomc.go.tz)) NA**

**MITANDAO RASMI YA KIJAMII YA HALMASHAURI (ubungomanispaa)  
WANANCHI WANaweza KURUDUFU NAKALA HIZO NA KUWASILISHA MAONI  
NDANI YA SIKU HIZO 14.**

**NYOTE MNAKARIBISHWA**

.....

**BEATRICE R. DOMINIC  
MKURUGENZI WA MANISPAA  
HALMASHAURI YA MANISPAA YA UBUNGO**